SEHEMU A

ZOEZI 1A: MAZUNGUMZO YA ANA KWA

ANA Maagizo maalum

i. Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.

ii. Mwamkue na kumwomba akae.

iii. Jitambulishe kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu_____'.

iv. Muulize jina lake.

v. Anza tathmini kwa kusema,

'Leo ningependa tuzungumze kuhusu shughuli ambazo watu hufanya kujipatia mapato.

5. Je, mzazi au mlezi wako anafanya shughuli gani ili kujipatia mapato ?

(Mwanafunzi ajibu)

6. Hebu nieleze, mapato anayopata yanamfaa vipi?

(Mwanafunzi ajibu)

3. Ukimaliza masomo ungetaka kufanya shughuli gani maishani ili kujipatia mapato? Nieleze sababu za kuchagua shughuli hiyo.

(Mwanafunzi ajibu)

i. Umeshinda mbio za riadha shuleni mwenu. Umepewa kuku kama zawadi. Utafanya nini ili upate manufaa kutokana na zawadi hiyo?

(**Mwanafunzi ajibu)**